



SADERA

**KILELE CHA MAADHIMISHO YA WIKI YA
UNYONYESHAJI DUNIANI**

7 AGOSTI, 2018

KATA YA HERUJUU

KAULI MBIU

**“UNYONYESHAJI WA
MAZIWA YA MAMA
NI MSINGI WA
MAISHA.”**

**HALMASHAURI YA MJI KASULU
MAADHIMISHO YA WIKI YA UNYONYESHAJI DUNIANI
TAARIFA FUPI KWA MGENI RASMI**

1. UTANGULIZI:

Tarehe 7 Agosti ya kila mwaka ni kilele cha kukamilisha wiki iliyotengwa na umoja wa mataifa katika kuadhimisha wiki ya Unyonyeshaji. Wiki hii kwa ujumla ni wiki ya kukumbushana wale wote wanaonyonyesha kuwa ni vema kuzingatia taratibu zote zinahusu kanuni za unyonyeshaji ili kuweza kujenga Afya kwa watoto.

Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama ina umuhimu mkubwa sana katika kuzuia aina zote za utapiamlo kwa watoto. Madhumuni ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani ni:

- Kujenga uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa unyonyeshaji na Ulishaji sahihi wa watoto wachanga na wadogo katika uhai na maisha yao.
- Kuihabarisha jamii ni kwa jinsi gani unyonyeshaji ni muhimili mkuu katika kuzuia utapiamlo kwa watoto.
- Kuhamasisha jamii kuhusu kusaidia wanawake wote waweze kunyonyesha watoto wao ipasavyo.
- Kushirikisha wadau mbalimbali katika kuendeleza, kulinda na kusaidia unyonyeshaji wa maziwa ya mama.

Kwa kawaida, Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani yamekuwa yakibeba jumbe tofauti kila mwaka, zinazolenga katika kulinda, kuendeleza na kusaidia unyonyeshaji wa maziwa ya mama. Kwa mwaka huu 2018, ujumbe mahususi wa maadhamisho haya ni **“UNYONYESHAJI WA MAZIWA YA MAMA NI MSINGI WA MAISHA.”** Kauli mbiu ya mwaka huu 2018 inalenga katika kusaidia kufikia malengo ya maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2030. Kimsingi kaulimbiu hii inahimiza umuhimu wa unyonyeshaji katika kuzuia aina zote za utapiamlo ili kuwa na rasilimali watu imara ambayo inahitajika ili kufikia maendeleo ya taifa kwa ujumla.

2. UMUHIMU WA UNYONYESHAJI

Kama tunavyofahamu unyonyeshaji wa maziwa ya mama huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha afya, kulinda uhai na maisha ya mtoto. Kunyonyesha maziwa ya mama pekee katika miezi sita ya mwanzo ya maisha ya mtoto ndio njia bora na salama ya kumpatia mtoto virutubishi vyote muhimu kwa ukuaji na maendeleo yake. Maziwa ya mama yana sifa ya kipekee ya kuwa na kinga mwili ambazo humkinga mtoto dhidi ya magonjwa mbali mbali hivyo kuchangia katika kupunguza vifo vya watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano. Tendo la kunyonyesha pia linajenga mahusiano kati ya mama na mtoto wake hivyo kumjenga mtoto kijamii zaidi. Wataalam wa Afya wanashauri kuwa Mtoto anapofikia umri miezi sita, anapaswa kuanzishiwa vyakula vya nyongeza, lakini aendelee kunyonyeshwa maziwa ya mama mpaka atimize miaka miwili au zaidi. Unyonyeshaji una mchango mkubwa katika kupunguza magonjwa yasiyoambukiza.

3. TAKWIMU CHACHE JUU YA HALI YA UNYONYESHAJI KATIKA HALMASHAURI YA MJI.

Takwimu hizi zimepatikana katika vituo vya tiba kwa mama waliofika ili kupata huduma zingine za afya kwa watoto wao.

Mwaka 2017 Watoto waliokuwa chini ya umri wa miezi 6 na wakiwa wanaendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama tu ni watoto 53,834 na wale wachanga wanaoendelea kupata maziwa mbadala ni 1,683

4. MAFANIKIO:

Yapo mengi ya kujivunia kufanyika kwa siku hii ya unyonyeshaji duniani lakini kwa ufupi naomba kutaja haya machache:-

- ✓ Elimu ya afya juu ya unyonyeshaji wa maziwa ya Mama pekee imeendelea kutolewa tangu siku ya uzinduzi, kupitia vituo vyetu ya tiba.
- ✓ Bado akina Mama wanaotii maagizo haya wanaendelea kuwanyonyesha watoto wao inavyopaswa, yaani hadi mtoto anapofikisha miaka 2.

5. CHANGAMOTO:

- I. Imani potofu miongoni mwa akina mama wanaonyonyesha hasa wanapopata ujauzito wakiwa bado watoto wao wananyonyeshwa kuwa watapata wanaharisha na kudumaa.
- II. Akina mama kukosa muda wa kutosha wa kuwanyonyesha watoto wao kutokana na kukabiliwa na shughuli za kutafuta maisha.

6. USHAURI KWA UMMA JUU YA UNYONYESHAJI:

- ✓ Mama wanaonyonyesha wapunguziwe kazi za kufanya ili wawe na nafasi ya kuweza kunyonyesha watoto wao, hii pia tunaomba kwa akina Baba kuwasaidia Kazi za kufanya Mama wanaonyonyesha ili wawe na muda mwingi wa kumnyonyesha Mtoto.
- ✓ Ikitokea Mama amepata ujauzito wakati alikuwa akiendelea kumnyonyesha mtoto, asisite kuendelea kumnyonyesha mwane hadi hapo ujauzito wake utakapotimiza umri wa miezi 7.
- ✓ Mtoto aendeleo kunyonyeshwa maziwa ya Mama pekee hadi atakapokuwa ametimiza umri wa miezi 6 atakapoanzishiwa vyakula vya nyongeza.
- ✓ Mama wanaonyonyesha waendeleo kupata mlo wa kutosha na unaozingatia makundi matano ya vyakula ambayo ni nafaka, nyama na na jamii yamikunde, mbogamboga, Matunda na vyenye mafuta na sukari.

7. SHUKURANI:

Tunatoa shukurani kwa wote walioshiriki siku hii ya leo wananchi na wadau mbalimbali wa wamendeleo kwa kufanikisha shughuli hii. Kwa kuwataja wachache ni pamoja na SADERA Kasulu kwa masaada wa maandalizi haya, Radio Kwizera kwa ushiriki wao, Viongozi wa Kata ya Herujuu, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mji Kasulu na Ofisi ya Mkurugenzi. Kwa ujumla wenu wote tunatoa shukurani na asanteni kwa kunisikiliza.